# AFYA YA IKOLOJIA.

RICHARD MHINA, **Country Director**
+255 715 858 354 | +255 767 858 354
NSSF New Building, 9th Floor, P.O. Box 7764, Moshi, Tanzania. www.floresta.co.tz
MOSHI | SAME | ROMBO | SIHA | HAI | MWANGA

Floresta
TUIPONYE ARDHI NA WATU WAKE

# AFYA YA IKOLOJIA.

## 1. UTANGULIZI

### 1.1. Maana ya Ikolojia.

Ikolojia – Ni jumuiya ya viumbe hai ( Mimea na Wanyama) pamoja na vipengele visivyo hai vinavyowazunguka (Mfano; Hewa, Maji, Madini) vyote kwa pamoja vikiishi, kuingiliana na kushirikiana kwa pamoja kama mfumo**.**

### 1.2. Maana y Afya ya Ikolojia.

Ikolojia yenye afya inajumuisha mimea ya asili/asilia pamoja na makundi ya wanyama wakubwa kwa wadogo, wanaoonekana kwa macho na wasioonekana kwa macho kwa pamoja vikiingiliana katika uwianao sawia na viumbe visivyo hai.

Mfano; Maji, Hewa na Udongo(Miamba)

**Namna mwingiliano unavotokea:**

- Ikolojia yenye afya ina chanzo cha nishati; mara nyingi ambacho ni Jua, lakini Jua likizidi huathiri mimea (Miti).
- . Jua hutoa nishati ya mwanga ambayo hutumiwa na wazalishaji (Mimea) kwa ajili ya ukuaji.
- Wazalishaji (Mimea) hubadili nishati ya jua kuipeka kwenye Nishati ya kikemikali ili waweze kuitumia wenyewe na pamoja na watumiaji ( Wanyama) i.e chakula cha wanyama.
- Walaji/ watumiaji (Wanyama) hula wazalishaji (Mimea) ambao baadae hurejesha virutubisho kwenye udongo.
- Walaji wakubwa (Wanyama wakubwa) hula wanyama wengine wadogo; nao pia husaidia kuongeza rutuba/virutubisho kwenye udongo.
- Bacteria, fungus, protozoa huvunja vunja mimea iliyokufa na wanyama na kurejesha virutubisho muhimu kwenye udongo.

- Mimea huchukua/hufyonza hivi virutubisho pamoja na maji kupitia mizizi ma kutengeneza chakula chake.

**Vipengele vya Ikolojia yenye Afya.**

**Ikolojia yenye Afya hujumuisha vipenegele vifuatavyo;**

- Mwanga wa Jua (chanzo cha nishati)
- Viumbe hai (wazalishaji, walaji, wavunjaji; wawindaji/wawindwaji)
- Viumbe visivyo hai ( milima na mabonde, vyanzo vya maji, miamba)
- Viumbe waliokufa ( mizoga)·
- Mipaka asilia – inayotengenezwa na viumbe hai na visivyo hai ndani ya eneo husika, Mfano: Vyanzo vya maji, Misitu, Milima n.k

**Namna maisha yanavotegemea Ikolojia.**

Maisha yanategemea Ikolojia kupitia huduma zifuatazo;

- Hewa safi,
- Maji safi,
- Chanzo cha nishati ( mfano Kuni),
- Madawa,
- Zana za ujenzi,
- Kupata chakula,
- Uratibu wa magonjwa mbalimbali (disease regulation),
- Uratibu wa hali ya hewa (climate regulation),
- Utosherevu wa kiroho,
- Furaha ya kuona uzuri wa eneo Fulani/ kivutio.
- Faida za mapumuziko ya kiutalii- hasa kwa watu ambao wanaweza kumudu gharama.

2. **Kwa nini Shirika la Floresta tunahamasisha wa Afya ya Ikolojia.**

   Tunahamasisha urejeshwaji wa afya ya Ikolojia kwa sababu tunajua kwamba, Dhana/wazo la Afya ya Ikolojia halijumuishi tu sehemu ya viumbe

hai na visivyo hai ndani ya Ikolojia, bali uchumi-jamii, tamaduni, afya ya binadamu na hali ya utawala wa jamii ya mwanadamu ambavyo kwa pamoja hutengeneza sehemu ya Ikolojia.

Kwa kutumia mbinu ya Afya ya Ikolojia kwenye suala la maendeleo endelevu**,** hivyo huhitaji tathimini ya Afya ya Ikolojia ambayo huleta uhusiano kati ya Kibaolojia, Afya ya binadamu, thamani ya tamaduni na kipato endelevu.

Hata hivo, hizi sifa zote huwa sio mara zote huwa katika mstari mnyoofu. Uvunaji mkubwa wa bidhaa za mazingira inaweza kuongeza faida za jamii-uchumi kwa muda mfupi na kuboresha afya ya binadamu kwa baadhi ya Nyanja za jamii husika lakini baaade huleta/ husababisha Uharibifu mkubwa wa mazingira.

Kwa kipindi cha muda mrefu, uharibifu endelevu wa Ikolojia huleta madhara hasi kwa afya ya binadamu na hali ya kiuchumi na inaweza hatarisha uendelevu wa kipata cha Jamii (kama uharibifu wa Ikolojia ukizidi uwezo wake wa kujirejesha kwenye hali iliopotea).

Lakini pia, tunahamasisha Afya ya Ikolojia kwa sababu ; kurejesha Ikolojia ndani ya eneo lililoathiria na uharibifu wa mazingira husaidia pia kurudisha bioanuai za dunia zilizopotea, ikiwa ni pamoja na kurejesha huduma za Ikolojia. Mfano wa huduma za Ikolojia ni Kuboresha ubora wa maji na Kufyonza hewa ya ukaa huduma amabazo humunufaisha maisha ya mwanadamu.

**3. Namna shughuli za Floresta zinavosaidia kurejesha Afya ya Ikolojia.**

Ufufuaji wa Afya ya Ikolojia – Ni kitendo cha kuanzisha na kurejesha Ikolojia zilizo haribiwa, makazi ya wanyama kwenye mazingira kwa kushirikisha mwanadamu.

Sisi kama Floresta tuna shughuli nyingi ambazo husaidia kurejesha Afya ya Ikolojia; Ambazo ni;

- Kuotesha miti ( Hasa miti ya asili kwa sababu huvumilia hata hali ngumu ya kimazingira mfano Ukame).
- Kufanya usafi (Uhifadhi wa vyanzo vya maji kwa kuweka uzio, kuotesha miti,).
- Kilimo hai ( Matumizi ya mbolea za wanyama, mimea rafiki na madawa ya asili).
- Kufundisha juu ya matumizi ya matumizi ya nishati mbadala/majiko banifu ( Hupunguza matumizi ya mkaa kama chanzo cha nishati).
- Utowaji wa zawadi (hii hujumuisha mafunzo) ya miradi ambayo husaidai wanufaika kuwa na vyanzo vingi vya kipato mfano, mradi wa mbuzi, mradi wa nyuki, mradi wa kuku. Tunafanya yote haya tukiamini kwamba kama mtu ana chanzo cha kipato Zaidi ya kimoja ,kiwango cha uharibifu wa mazingra hupungua kwa kiasi kikubwa.

**4. Uumbaji wa Mungu na Ikolojia.**

Ikolojia ni kitu cha neema kuliko tunavyojua. Mungu alituumba ili tukae katika mahusiano mazuri baina yetu na vyote vinavyoijaza dunia. Ikolojia hufanya kazi kama kiashiria cha Dunia kwamba- usawa kwenye uhifadhi wa dunia husaidia watu wa Mungu kuishi na kupiga hatua kimaendeleo. Tunapofanya kinyume na uumbaji wa Mungu – mahusuiano yetu hudhoofika.

Hapo mwanzo Mungu aliuumba Ulimwengu na ndani yake sayari inayoitwa Dunia. Baadae alimuumba mwanadamu na kumpa jukumu kuu kuhifadhi Sayari (Mwanzo 2:15)

Vitendo vyote ni sehemu ya mwendelezo ambao umepelekea keleta matokea. Kwa sababu hii, Mungu anatuamulisha sote kuwa makini na yote

tunatendayo (Kumbukumbu la torati 32:29). Pia tunaagizwa kufanya mipango ya mbele ( Wakorintho 12:14)- hii itatusaidia sote tunavyotekeleza neno muhimu kutoka kwa Mungu; agizo la kutunza Ulimwengu unaotuzunguka ( Mithali 12:10)

Leo, tunaona kwamba matendo yetu yamesababisha uharibifu mkubwa kwenye uso wa dunia. Katika Ikolojia ya Mungu, Dunia na vyote viijayo vilikuwa vinahusiana – lakini kwa sasa Mabadiliko ya hali ya hewa yanaumiza/kuathiri watu wa Mungu.

Katika mzunguko wa maisha asilia- kemikali zilizo hewani hufyoonzwa na mimea ambayo ni chanzo cha chakula kwa bindamu na viumbe wengine. Lakini hizi kemikali zilizo hewani ni mbaya, hewa na chakula siyo salama kwa matumizi ya binadamu.

Sheria na maagizo yaliyo tolewa na Mungu ni kwa ajili ya utashi kiroho na mwonekano wa mwanadamu. Tunaaagizwa hivo katika kitabu cha Deuteronomy, Sura 10, mstari wa 13. Na kama tutafuata hizo sheria, itasaidia Ikolojia kurejea katika hali yako, Dunia na wote wanaoiita masikani mwao wataneemeka./pendeza.